# HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 26/11/2021**

**KUMB. NA. 13/2021/2022 – WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Nd. Salum Mpili | - Afisa Mipango (W) | -Mwenyekiti |
| 2. Nd. Mawazo Mbunda | -Afisa Ugavi (W) | -Katibu |
| 3. Nd. Mahmoud Kimbokota | -Afisa Utumishi (W) | -Mjumbe |
| 4. Nd. Abruhani O. Juma | -Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) | -Mualikwa |
| 5. Nd. Alphonce Ngongi | -Afisa Uchaguzi (W) | -Mjumbe |
| 6. Nd. Msafiri D. Wanje | -Kaimu Mwanasheria (W) | -Mualikwa |

**KUMB. NA. 13.2/2021/2022 – WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA:**

| | |
|---|---|
| 1. Nd. Violeth Byanjweli | -Afisa Kilimo na Ushirika |
| 2. Dr. Dismas Masulubu | - Mganga Mkuu (W) |

**KUMB. NA. 14/2021/2022 – KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao cha dharula cha Bodi ya zabuni kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na aliwataka wajumbe kujadili agenda zilizowasilishwa kikaoni kwa umakini.

Alifungua kikao saa 03.15 asubuhi.

**KUMB.NA. 15/2021/2022 – KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI YA "FORCE ACCOUNT" UJENZI WA MAJENGO YA HOSPITALI YA WILAYA KIWALALA PAMOJA NA NYUMBA YA WATUMISHI.**

Katibu wa Bodi ya Zabuni aliwasilisha kikaoni taarifa ya mapokezi ya fedha shilingi Milioni Mia Nane Tisini (890,000,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa majengo manne kwa shilingi (800,000,000/=) milioni mia nane ambayo ni jengo la upasuaji, wodi ya upasuaji ya wanaume, wodi ya upasuaji ya wanawake na jengo la kuhifadhia maiti (mortuary) na shilingi milioni tisini (90,000,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi familia tatu kwa moja (3 in 1 house) katika Hospitali ya Wilaya Kiwalala.

Awali muendelezo wa ujenzi huu wa majengo manne katika mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 ulipangiwa kutumia njia ya manunuzi ya "restricted tendering" kwa mantiki hiyo Kitengo cha Manunuzi kinapendekeza kubadilisha njia hiyo na kuendelea na utaratibu wa "force account" ambao ulianza kutumika kwa majengo ya awali.

Hivyo Kitengo cha Manunuzi na Ugavi sawa na ibara namba 167 ya kanuni ya manunuzi ya mwaka 2013 kinapendekeza ujenzi huu ufanyike kwa njia ya "force account" kwa



Scanned with CamScanner

maana ya kwamba mchakato wa manunuzi utafanywa na kamati ya ujenzi ya Hospitali ya Wilaya.

Wajumbe kwa pamoja baada ya kupitia taarifa ya mapokezi ya fedha za ujenzi wa majengo ya upasuaji, jengo la kuhifadhia maiti na nyumba ya mtumishi "3 in 1" waliridhia mabadiliko ya njia ya manunuzi ya "restricted tendering" iliyopangwa kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 na kuamua ujenzi wa majengo hayo yote kwa ujumla wake yajengwe kwa kutumia njia ya manunuzi ya "force account".

**KUMB.NA. 16/2021/2022 – KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI YA KUMPATA MTAALAMU MSHAURI WA KUSANIFU NA UCHORAJI WA RAMANI YA KITUO CHA MABASI MTAMA.**

Katibu wa Bodi ya Zabuni aliwasilisha kikaoni barua ya maombi ya kuanza mchakato wa Kumpata mataalam mshauri wa kufanya usanifu na uchoraji wa ramani ya kituo cha mabasi Mtama.

Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kilishauri kutumia njia ya manunuzi ya "National Competitive selection"sawa na kanuni ya manunuzi namba 255 ya mwaka 2013, ambapo njia hii inawezesha upatikanaji wa maandiko "proposal" toka kwa wataalam washauri mbalimbali kwa lengo la kupata ushindani.

Katibu wa Bodi ya Zabuni aliwasilisha kikaoni nyaraka ya zabuni ya kumpata mtaalam mshauri wa kufanya usanifu na uchoraji wa ramani ya kituo cha mabasi Mtama kwa ajili ya kuipitia na kuidhinisha ili iweze kutumika katika mchakato wa zabuni hii.

Wajumbe kwa pamoja waliridhia matumizi ya njia ya manunuzi ya "National Competitive selection" na kuidhinisha nyaraka ya zabuni ya kumpata mtaalam mshauri wa kufanya usanifu na uchoraji wa ramani ya kituo cha mabasi Mtama.

**KUMB.NA. 17/2021/2022 – KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI YA "FORCE ACCOUNT" UJENZI WA UMALIZIAJI WA MABOMA KATIKA ZAHANATI ZA CHIUTA, MBAWALA, MTEGU NA CHIWERERE.**

Katibu wa Bodi ya Zabuni aliwasilisha kikaoni taarifa ya mapokezi ya fedha shilingi Milioni Mia Mbili Tu (200,000,000/=) kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati nne (4) ambazo ni Chiuta, Mbawala, Mtegu na Chiwerere ikiwa mgao wake kila Zahanati imepatiwa shilingi 50,000,000/= (Milioni Hamsini).

Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kilipendekeza ukamilishaji huo ufanyike kwa njia ya "force account" sawa na ibara namba 167 ya kanuni ya manunuzi ya mwaka 2013 na mchakato wa manunuzi ufanywe na kamati zilizopo ngazi ya kituo.



Scanned with CamScanner

Wajumbe kwa pamoja baada ya kupitia taarifa ya mapokezi ya fedha za ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya zahanati nne (4) ambazo ni Chiuta, Mbawala, Mtegu na Chiwerere waliridhia ukamilishajiukamilishaji huo utekelezwe kwa njia ya "force account" sawa na ibara namba 167 ya kanuni ya manunuzi ya mwaka 2013 na mchakato wa manunuzi ufanywe na kamati zilizopo ngazi ya kituo.

**KUMB.NA. 18/2021/2022 – KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI YA "FORCE ACCOUNT" UJENZI WA MADARASA KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI.**

Katibu wa Bodi ya Zabuni aliwasilisha kikaoni taarifa ya mapokezi ya fedha shilingi Bilioni Moja Milioni Mia Moja Sitini Tu (1,160,000,000/=) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa madarasa kwa shule za msingi na sekondari. Shule 12 za sekondari zitatumia shilingi 760,000,000/= na shilingi 400,000,000/= kwa shule 5 za msingi. Halmashauri ya Wilaya Mtama itatekeleza ujenzi wa madarasa 58 kati ya hayo 38 ya shule za sekondari na 20 ya shule za msingi. Fedha hizi za ujenzi za uviko 19 zimepelekwa mashuleni ambapo kila darasa limetengewa shilingi 20,000,000/= za ujenzi.

Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kilishauri njia hii ya manunuzi ya "force account" sawa na ibara namba 167 ya kanuni ya manunuzi ya mwaka 2013 itumike na kamati za ujenzi zilizopo vituoni ili kuharakisha utekelezaji wa ujenzi wa madarasa. Pia Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kilipendekeza kwa Bodi ya Zabuni iidhinishe fedha hizi ziingizwe kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 kwa kuwa zimekuja nje ya bajeti.

Wajumbe kwa pamoja baada ya kupitia taarifa ya mapokezi ya fedha za ujenzi wa madarasa wote kwa pamoja waliridhia ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari kujengwa kwa kutumia njia ya manunuzi ya "force account" na utekelezaji wake ufanywe na kamati za ujenzi zilizopo vituoni, pia wajumbe waliridhia fedha za ujenzi wa madarasa ziingizwe kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022.

**KUMB. NA. 19/2021/2022 KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 05.10 asubuhi akiwashukuru wajumbe kwa kujadili kwa umakiniajenda zilizowasilishwa kikaoni.

**UMETHIBITISHWA**

.......................................... ..........................................

**KATIBU** **MWENYEKITI**

**TAREHE** 25/01/2022



Scanned with CamScanner